# SHINDANO

## La Insha na Mdahalo



### Kwa Shule za Upili
### Eneo La Afrika Mashariki

*(Zikiwemo nchi za Burundi na Rwanda)*

## MADA: WEKA AKIBA, UEKEZE ILI UKUZE UCHUMI

## Kuhusu Shindano hili

Shindano hili ni la Tatu kuandaliwa na shirika la IREN (Inter Region Economic Network) tangu mwaka 2006. Lengo lake ni kukuza lugha ya Kiswahili pamoja na kueneza mikakati ya kuimarisha uchumi. Shindano hili ni wazi kwa wanafunzi wote wa shule za upili katika nchi za Tanzania, Uganda, Rwanda, Burundi na Kenya. Mwaka huu, washindiwatashiriki kwenye mafunzo maalum ya biashara na uongozi.

## Jinsi Ya Kushiriki

Tuma insha fupi kuhusu mada "Kuza uchumi kwa kuweka akiba" ukieleze kwa kinaga ubaga sababu za kushiriki kwenye mdahalo huu. Washiriki watume insha zao kupitia ofisi ya mwalimu mkuu wa shule zao na kutufikia kabla ya tarehe 25 Mei 2009. Insha bora zitachaguliwa na washiriki kuombwa kuhudhuria Mdahalo wa kitaifa ili kutetea hoja zao mnamo tarehe 15 Juni 2009.

## Tuzo

Mshindi atatuzwa shilingi za Kenya 10,000 na shule yao kuzawadiwa vitabu kuhusu uchumi wa soko. Washiriki wote watakaofuzu kuhudhuria mdahalo watatunukiwa zawadi mbali mbali. Washindani ni sharti wahakikishe kuwa insha zao zina nambari zao za usajili shuleni pamoja na mihuri rasmi wa shule.

Kwa maelezo zaidi, mpigie Anne simu kupitia nambari + 254 020 2731497
au Andika barua pepe kwa anwani: events@irenkenya.com

## Ratiba

| Tarehe/ Siku | Funzo/ Mada | Msimamizi |
|---|---|---|
| 15.Juni.2009 | Mdahalo | Bi. Anne Mugoya (Kenya) |
| 16.Juni.2009 | Biashara | Bi. Lena Zamchiya (Zimbabwe) |
| 17.Juni.2009 | Uongozi | Bw. James Shikwati (Kenya) |
| | | |
| | | |

Shindano Hili Limedhaminiwa na:

IREN Inter Region Economic Network — Kenya

SIFE — Kenya

The BOOST Fellowship — Zimbabwe

Tuma Insha kwa: Mwandalizi Msimamizi
Inter Region Economic Network Jumba la Nyaku,
Hurlingham. S.L.P. 135 - 00100, Nairobi - Kenya